

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINNGWEA SHULE YA SEKONDARI MBONDO**

SIMU. 0736983242  
0620804426



S.L.P 129,  
**NACHINGWEA.**

**KUMB. NA. MB/SS/AD/01/20**

14/12/2020

JINA LA MWANAFUNZI.....

SHULE YA MSINGI .....

NAMBA YA MTIHANI .....

## **YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA MBONDO KIDATO CHA KWANZA MWAKA - 2021**

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2021.

Masomo atakaojifunza ni pamoja na

- |  |             |               |                 |
|--|-------------|---------------|-----------------|
| (a) Kiswahili                            | (b) Uraia   | (c) Jiografia | (d) Historia    |
| (e) Kemia                                | (f) Fizikia | (g) Baiolojia | (h) Kiingereza. |
| (i) Hisabati na masomo mengine ya ziada. |             |               |                 |

Ili kujifunza masomo yote kwa urahisi atatakiwa kutumia lugha ya kiingereza wakati wote awapo shulenii.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shulenii tarehe hiyo ili asajiliwe

Mwisho, pamoja na barua hii naambatanisha viambata A, B C na D. Mzazi/mlezi yakupasa usome, uelewe na kutekeleza ili katuondolea usumbufu hapo baadae

***“KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MBONDO”***

.....  
**ALEX MSHOTTA  
KAIMU MKUU WA SHULE**

### **NAKALA:**

1. Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya (W) Nachingwea  
S.L.P 291,  
NACHINGWEA

## **1.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

- (i) Ili mwanaao aweze kupokelewa shulenii, maagizo yaliyobainishwa katika barua hii lazima yatekelezwe.
- (ii) Usipomleta mwanaao kwa wakati, utapelekwa mahakamani kwa shitaka la kumtorosha mwanaao

### **A. SARE ZA SHULE**

- **WAVULANA**

- (i) Suruali mbili za kushona zenyne mfuko mmoja wa nyuma, (Isiwe muundo wa jinzi, ama akudo, Ngwasuma) rangi blue bahari
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
- (iii) Viatu jozi mbili vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe
- (iv) Awe na mkanda wa ngozi au plastiki wa rangi nyeusi pamoja na fulana inayopatikana shulenii kwa gharama zako

- **WASICHANA**

- (i) Sketi mbili za blue bahari ndefu zinazofunika magoti (rinda box)
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi au nusu kanzu kwa mwanafunzi muislamu pamoja na hijab ifanane na rangi ya shati au nusu kanzu.
- (iii) Viatu jozi mbili vyeusi vya kutumbukiza vya ngozi vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe pamoja na tisheti inayopatikana shulenii kwa gharama zako
- (iv) Viatu vya shule tunashauri vinunuliwe vya mtumba kwani vinadumu kwa muda mrefu
- (v) Waje na chandarua (neti ya mbu)

### **B. VIFAA VYA USAFI NA KILIMO**

Hakikisha kijana anakuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi na kilimo:-

- (i) Jembe (Ngwamba) lenye mpini
- (ii) Fagio na ndoo
- (iii) Fyekeo kwa wasichana
- (iv) Panga kwa wavulana

Atutapokea mwanafunzi asiye na vifaa vya usafi

### **C. VIFAA VYA MICHEZO**

- (i) Tracksuit rangi ya bluu jozi moja na viatu (raba)
- (ii) T-shirt zinapatikana shulenii kwa gharama ya mzazi

### **D. VIFAA VYA TAALUMA KWA AJILI YAKE**

- (i) Daftari kubwa kumi (10)
- (ii) Faili moja la kutunzia kumbukumbu zake muhimu
- (iii) Kamusi ya Kiingereza kwa Kiswahili (Dictionary) zinapatikana shulenii kwa gharama zako
- (iv) Mkebe wenye vifaa vya Hisabati
- (v) Begi ya kubebeara daftari (mfuko wa Rambo marufuku)
- (vi) Rim moja ya karatasi

## **E. MAHITAJI YA CHAKULA**

Shule inaendesha mpango wa chakula kwa wanafunzi wote kwa milo yote inayoghamiwa na wazazi kwa kulipa kiasi cha fedha Tsh 250000/= kwa mwaka au Tsh 125000/= kwa mhula kupitia akaunti **70406600038** (mfuko wa maendeleo ya kata mbondo) .

**NB** Mwanafunzi/mzazi/mlezi anatakiwa kufika na risiti ya benki shule itakapo funguliwa kwa ajili ya kujiridhisha malipo yake kwa mwasibu . Hata hivyo mzazi au mlezi ikumbukwe suala la michango ya chakula ni jukumu lako hivyo unapaswa kuchangia.

## **2.0. MAMBO MENGINE MUHIMU ANAYOPASWA KUWA NAYO MWANAFUNZI AWAPO SHULENI**

- (a) Fomu ya daktari, ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali.
- (b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
- (c) Kitambulisho cha bima ya afya ya jamii (CHF au NHIF), kama hana atatoa Tsh. 5,000/= kwa ajili ya Bima ya Afya iliyoboreshwa.

## **3.0. UTAMBULISHO WA MZAZI- KATA ULETE SHULENI**

Jina la Baba (matatu) ..... (Hai / Amekufa)

Jina la mama (matatu) ..... (Hai/ Amekufa)

Jina la mlezi (kama huna wazazi) majinamatatu .....

Kitongoji anakoishi Mzazi / Mlezi .....

Namba ya simu ya Mzazi / Mlezi.....

Namba ya simu ya Mwenyekiti wa kitongoji .....

**SAHIHI YA MZAZI / MLEZI .....**

## **I. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 Aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Pamoja na Ofisi ya Rais – Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- (i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- (ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba za shule ni lazima
- (iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (iv) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- (v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- (vi) Kuva sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (vii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (viii) Kutunza mali za Umma
- (ix) Viduku na unyoaji wa mitindo hauruhusiwi shuleni

## **II. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- (i) Wizi
- (ii) Uasherati na ushoga
- (iii) Ubakaji
- (iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli n.k
- (v) Kupigana au kupiga
- (vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
- (vii) Kudharau bendera ya Taifa
- (viii) Kuwa mjamzito / kupata mimba
- (ix) Kuoa au kuolewa
- (x) Kutoa mimba au kusabisha mimba ndani na nje ya shule
- (xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (xii) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (xiii) Kuwa na simu ya mkononi.

*Kiambatisho "C"*

**MBONDO SECONDARY SCHOOL**  
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**FROM:**

THE HEADMASTER,  
MBONDO SECONDARY SCHOOL,  
P.O.BOX129,  
NACHINGWEA  
14/12/2020

**TO:**

DISTRICT MEDICAL OFFICER  
NACHINGWEA GOVERNMENT HOSPITAL,  
P.O.BOX 30,  
NACHINGWEA.

**RE; STUDENT'S FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical officer in respect of all students from school

1. Full student's name.....
2. Age ....., Sex ....., Years.....
3. Blood count (red and white).....
4. Stool examination.....
5. Urinary system.....
6. Syphilis.....
7. Venereal disease test.....
8. T.B Test.....
9. Eye Test.....
10. Ears.....
11. Chest.....
12. Spleen.....
13. Abdomen.....
14. Urine for plan test.....

Additional information (if any) e.g. physical defect or impairment(s) e.g. arm, leg, etc infections, chronic of family diseases etc.

I have examined the above named student and certify that she/he is physically or mentally fit/unfit for full course of secondary Education

Signature.....

Designation.....

## *Kiambatisho “D”*

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**  
**SHULE YA SEKONDARI MBONDO**

# FOMU YA WAZAZI AU WALEZI

Tafadhalii andika hapa chini orodha ya marafiki na jamaa ambao wanaweza kumtembelea kijana wako shulenii, ambao wanaruhusiwa kuwatembelea nyumbani kwao wakati wa Likizo fupi au ndefu.